# JARIDA LA

WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

*Wizara ya Furaha*

**Toleo Maalum la: 20** | 29 Juni, 2021 | www.habari.go.tz

# MASHINDANO YA NGOMA ZA ASILI UMISSETA 2021 YAHITIMISHWA RASMI



# YALIYOJIRI KATIKA WA MASHINDANO YA MICHEZO YA UMISSETA

29 Juni, 2021

**KAULIMBIU: "MICHEZO SANAA NA TAALUMA KWA MAENDELEO YA UCHUMI WA VIWANDA"**

# NUKUU YA MKURUGENZI WA IDARA YA MAENDELEO YA SANAA NCHINI DKT. EMMANUEL ISHENGOMA

Leo Juni, 29, 2021 mashindano ya UMISSETA kwa upande wa Kwaya na Ngoma yamehitimishwa ambapo washindi watatu upande wa Kwaya na watatu upande wa Ngoma watatangazwa muda wowote baada ya Waamuzi kujumlisha alama zao.

Washindi hawa watatu wamepatikana baada ya kushindanisha washindi wa awali 9 (watatu kutoka kila Mikoa 9).

Kupitia mashindano haya, wanafunzi wanapata fursa adhimu ya kujifunza uzalendo kupitia Wimbo Maalum.

Vilevile, vijana wanapata nafasi ya kuonesha na kujifunza tamaduni za Makabila ya Mikoa mbalimbali kupitia Ngoma ya Ndani ya Mkoa na Ngoma ya Nje ya Mkoa.

Pia tumeona vipaji binafsi kupitia kwa Manju na wapiga ngoma mbalimbali.

Jukumu kubwa tulilo nalo kama wasimamizi wa Sekta ni kuweka mfumo mzuri wa kuvuna vipaji hivi na kuviingiza katika Soko la ajira katika Sekta ya Sanaa.

Kwa kuanzia, nawaasa makampuni katika Sekta hii kuwa na utaratibu wa kuhudhuria mashindano kama haya na kutambua vipaji hivi na kuvitumia hasa baada ya masomo kwa maendeleo ya kiuchumi ya vijana wenyewe, kampuni husika na Taifa kwa ujumla.

Mwisho, wanafunzi, wanavyuo na wananchi waliopo Mtwara na maeneo ya jirani wanakaribishwa kishiriki Kilele cha Mashindano haya Juni 2, 2021 kwenye uwanja wa Nangwanda Sijaona

Nawahakikishia patachimbika kwa burudani kutoka kwa Washindi wa mashindano haya sambamba na wasanii maarufu wa kizazi kipya.



**DKT. EMMANUEL ISHENGOMA**

**Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Sanaa Nchini**

# ARUSHA, MANYARA MABINGWA MCHEZO WA RIADHA MITA 1500 UMISSETA 2021

Mikoa ya Arusha na Manyara imeongoza kwenye mchezo wa Riadha mita 1500 katika Mashindano ya Taaluma na Michezo kwa Shule za Sekondari (UMISSETA) kwenye fainali zilizofanyika leo Juni 29, 2021 mjini Mtwara.

Msemaji wa UMISSETA 2021, John Mapepele amesema kwa upande wa wavulana Daniel Patric kutoka Arusha ameibuka mshindi wa kwanza baada ya kumaliza mbio hizo kwa kutumia muda wa dakika 4:07:16 akifuatiwa na Paul Ndege kutoka mkoa wa Mara aliyetumia dakika 4:11:06 wakati nafasi ya tatu imechukuliwa na Agustino Leonard kutoka Mkoa wa Manyara aliyemaliza mbio hizo kwa dakika 4:12:44.

Kwa upande wa wasichana Leoma Awaki kutoka Manyara ameibuka mshindi wa kwanza baada ya kumaliza mbio hizo kwa kutumia muda wa dakika 4:44:50 akifuatiwa na Esther Martin kutoka mkoa wa Pwani aliyetumia dakika 4:46:80 wakati nafasi ya tatu imechukuliwa na Nyanzobe Mbahi kutoka Mkoa wa Mara aliyemaliza mbio hizo kwa dakika 4:49:66.

Wakati huo huo Mkoa wa Unguja kwa upande wa wavulana umeibuka mshindi wa kwanza katika mbio za kupokezana vijiti mita 4x100 (relay) kwa kutumia dakika (0:45:53), wakifuatiwa na mkoa wa Shinyanga (0:47:10), mkoa wa Tabora umeshika nafasi ya tatu (0:47:20), mkoa wa Pwani nafasi ya nne (0:48:53), mkoa wa Mara nafasi ya tano (0:50:91), na mkoa wa Dodoma umeshika mkia 0:51.09.

Kwa upande wa wasichana mkoa wa Njombe umeibuka mshindi wa kwanza katika mbio za kupokezana vijiti mita 4x100 (relay) kwa kutumia dakika (0:55:66), wakifuatiwa na mkoa wa Mara (B 0:56:16), mkoa wa Tabora umeshika nafasi ya tatu (0:56:19), mkoa wa Pwani nafasi ya nne (0:57:10) mkoa wa Simiyu nafasi ya tano (0:57:20) na mkoa wa Dodoma umeshika mkia (0:57:51).

# SHINYANGA MABINGWA MCHEZO WA KURUKA CHINI UMISSETA 2021

Mikoa ya Shinyanga na Pwani imeongoza kwenye mchezo wa kuruka chini katika Mashindano ya Taaluma na Michezo kwa Shule za Sekondari (UMISSETA) kwenye fainali zilizofanyika leo Juni 29, 2021 katika uwanja A kwenye chuo cha walimu mjini Mtwara.

Msemaji wa UMISSETA 2021, John Mapepele amesema Musa Yusufu kutoka Shinyanga ameibuka kuwa mshindi wa kwanza baada ya kuruka umbali wa mita 6 na sentimita 71 akifuatiwa na Mpaji Gipson kutoka mkoa wa kigoma aliyeruka umbali wa mita 6 na sentimita 35 wakati nafasi ya tatu imechukuliwa na Alexander Jumanne kutoka Mkoa wa Geita aliyeruka umbali wa mita 6 na sentimita 34.

Kwa upande wa wasichana Joha Mbaraka kutoka Mkoa wa Pwani ndiye Mshindi wa kwanza kwa kuruka mita 4 na sentimita 72 akifuatiwa na Witness Ibrahim kutoka Geita aliyeruka umbali wa mita 4 na sentimita 67 ambapo nafasi ya tatu ilichukuliwa na Diana Chacha kutoka Mara aliyeruka umbali wa mita 4 na sentimita 54.



Namshukuru Rais wangu kwa kututhamini sisi wasanii tunamwombea kwa Mungu azidi kutusaidia.

Tunatambua kuwa Sanaa kwa sasa ni mlango mzuri wa ajira.

Tutajitahidi kufanya vizuri ili ituingizie kipato.

**LUCAS NOEL NICHOLAUS**

**Mchezaji bora wa Ngoma za Asili - Mkoa wa Mtwara**

# MPIRA WA MIKONO WAVULANA

MASHINDANO YA UMISSETA MPIRA WA MIKONO KWA WAVULANA YAMEENDELEA LEO, JUNI 29, 2021. TIMU ZA MIKOA YA MOROGORO 24 (WENYE KIJANI) NA TANGA 13 (WENYE ZAMBARAU).





# MPIRA WA MIKONO WASICHANA

MASHINDANO YA UMISSETA MPIRA WA MIKONO KWA WASICHANA YAMEENDELEA LEO, JUNI 29, 2021. TIMU ZA MIKOA YA MBEYA 26 (WENYE BLUU) NA GEITA 27 (WENYE BLUU BAHARI)





# MPIRA WA KIKAPU WAVULANA

MASHINDANO YA UMISSETA MPIRA WA KIKAPU KWA WAVULANA YAMEENDELEA LEO, JUNI 29, 2021. TIMU ZA MIKOA YA MWANZA 88 (WENYE BLUU) NA RUKWA 17 (WENYE KIJANI).





# MPIRA WA WAVU WASICHANA

MASHINDANO YA UMISSETA MPIRA WA WAVU KWA WASICHANA YAMEENDELEA LEO, JUNI 29, 2021. TIMU ZA MIKOA YA TABORA 2 (WENYE BLUU) NA DAR ES SALAAM 3 (WENYE NYEUPE).





# MASHINDANO YA RIADHA
# KURUKA CHINI – WAVULANA

**MUSA YUSUFU KUTOKA SHINYANGA AMEIBUKA KUWA MSHINDI WA KWANZA BAADA YA KURUKA UMBALI WA MITA 6 NA SENTIMITA 71.**





# MASHINDANO YA RIADHA
# MBIO ZA KUPOKEZANA VIJITI – WAVULANA

## KUNDI LA WASHIRIKI KUTOKA PEMBA LIMEIBUKA KUWA WASHINDI WA KWANZA KWA MBIO ZA KUPOKEZANA VIJITI MITA 4 X 100 (RELAY).






# MASHINDANO YA RIADHA
# MBIO ZA KUPOKEZANA VIJITI – WASICHANA

## KUNDI LA WASHIRIKI KUTOKA NJOMBE LIMEIBUKA KUWA WASHINDI WA KWANZA KWA MBIO ZA KUPOKEZANA VIJITI MITA 4 X 100 (RELAY)






# MASHINDANO YA RIADHA
## MBIO ZA MITA 100 – WAVULANA

BENEDICTO MATHIAS MSHINDI MBIO MITA 100 WAVULANA.



# MASHINDANO YA RIADHA
# MBIO ZA MITA 100 – WASICHANA

## BENEDICTO MATHIAS MSHINDI MBIO MITA 100 WASICHANA.



# MASHINDANO YA RIADHA
## MBIO ZA MITA 1500 – WASICHANA

**LEOMA AWAKI MSHINDI MBIO MITA 1500 UPANDE WA WASICHANA.**



# MASHINDANO YA RIADHA
## MBIO ZA MITA 1500 – WAVULANA

### DAMIAN PATRICK MSHINDI MBIO MITA 1500 KWA WAVULANA.



# SANAA ZA NDANI
# NGOMA ZA ASILI

MASHINDANO YA UMISSETA UPANDE WA SANAA ZA NDANI (NGOMA ZA ASILI) YAMEISHA LEO, JUNI 29, 2021. MIKOA ILIYOSHIRIKI LEO NI LINDI, RUKWA, DODOMA, MWANZA, DAR ES SALAAM, PWANI, ARUSHA, NJOMBE NA MTWARA.



LINDI



MWANZA



DODOMA



RUKWA



DAR ES SALAAM



PWANI



ARUSHA



MTWARA



NJOMBE



ZANZIBAR

# UMITASHUMTA | UMISSETA 2021



## #MwakaWaVipaji

Limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo
S.L.P 25, 40470 DODOMA, TANZANIA